
# KUELEKEA LENGO



Kitabu Cha Watoto

## TIKETI YA DHAHABU

AMBASSADORS FOOTBALL

HABARI!

JINA LANGU NI FOOTY.

KARIBU KWENYE...

# KUELEKEA LENGO

HAPA NDIPO PA KUPATA KILA KITU...

HADITHI YA SOKA ukurasa wa 2
HADITHI YA BIBLIA ukurasa wa 5
KULINGANISHA HADITHI ukurasa wa 9
MASOMO ZA KUZINGATIA ukurasa wa 10
VIFUNGU VYA KUMBUKUMBU ukurasa wa nyuma

NATUMAINI UTAFURAHIA!



© 2025 Ambassadors Football. Haki Zote Zimehifadhiwa.

Ambassadors Football imeunda Kuelekea Lengo ili kutumiwa na watu wote duniani kote na bila malipo. Pia uko huru sambaza kwa wengine, kama ilivyo, bila madai ya umiliki. Huruhusiwi kutoza Kuelekea Lengo kwa njia yoyote ile au kuikusanya pamoja na bidhaa zingine ambazo zinauzwa au kupatianua.
Kuelekea Lengo lazima itumike kama ilivyo na haifai kuongezwa, au kupunguzwa, kwa namna yoyote.


Nyenzo za Kuelekea Lengo zinapatikana mtandaoni pamoja na nyenzo za kufundishia kwa wale ambao wangependa kuunda programu zao za huduma ya soka. Tafadhali tembelea tovuti kwa: www.ttgweb.org

Ikiwa na maswali yoyote au unahitaji msaada tafadhali wasiliana nasi kwa: ttg@ambassadorsfootball.org

Tafadhali tutembelee katika www.ambassadorsfootball.org ili kujifunza zaidi kuhusu huduma yetu ya kimataifa ya soka.


Manukuu ya Biblia:
Nukuu za Maandiko zenye alama (NIV) zimetolewa kutoka katika Biblia Takatifu, BIBLIA TAKATIFU, NEW INTERNATIONAL VERSION®, NIV® Hakimiliki © 1973, 1978, 1984, 2011 na taasisi ya Biblica, Inc.™ Imetumiwa kwa ruhusa. Haki zote zimehifadhiwa duniani kote. Nukuu za Maandiko zilizowekwa alama (NLT) zimechukuliwa kutoka katika Biblia Takatifu, Tafsiri ya New Living Translation, hakimiliki ©1996, 2004, 2015 na Taasisi ya Tyndale House. Imetumiwa kwa ruhusa ya Tyndale House Publishers, Carol Stream, Illinois 60188. Haki zote zimehifadhiwa. Nukuu za Maandiko zilizowekwa alama (GNT) zimetoka katika Tafsiri ya Habari Njema katika Toleo la Kiingereza la Today's English Version- Toleo la Pili Hakimiliki © 1992 na American Bible Society. Inatumika kwa Ruhusa. Maandiko yananukuu kutoka katika Biblia ya ESV® (Biblia Takatifu, Kiingereza Standard Version®), hakimiliki © 2001 by Crossway, huduma ya uchapishaji ya Good News Publishers. Inatumika kwa ruhusa. Haki zote zimehifadhiwa.

# TIKETI YA DHAHABU



Kombe la Kimataifa limefika Soccatown! Mashabiki kutoka kote ulimwenguni hujaa mitaani. Ni ndoto iliyotimia kwa Footy na marafiki zake.

Kila jioni, wanacheza mitaani na watoto kutoka nchi tofauti tofauti hujiunga nao! Mmoja wao anaitwa Grobb. Yeye ni mkubwa, mgumu, na kila wakati anatafuta kuanzisha shida. Hakuna mtu anapenda kucheza na Grobb!



Jerro anaita Footy akuje. Jerro ni mmoja wa wachezaji bora mjini nani mtoto wa mmiliki wa uwanja! Anampa Footy tiketi ya dhahabu - kiti katika uwanja kwa Fainali ya Kombe la Kimataifa! Footy hawezi kuamini! Jerro anatabasamu, "Baba yangu ndiye mmiliki wa uwanja na nina kiketi kathaa za bure za kumpa yeyote ninayemtaka!" Anamtazama Grobb akimsukuma mtoto mwingine.

"Footy, wachezaji bora sio wazuri tu uwanjani - wanajua jinsi ya kuwatendea watu vizuri vile vile, hata wale ambao wanawachukia ... utaona ninachomaanisha."




Wakati wa mechi kuanza umekaribia. Wengi wa umati tayari wako kwenye viti - Footy anachelewa kidogo, hakuweza kuchagua rangi za kuvaa! Alipofika mlangoni, anasikia sauti ya... Ni Grobb! Na yuko katika hali mbaya. Genge la watoto wakubwa lilikuwa likicheza vibaya. Sasa amelala barabarani na majeraha kwenye kifundo cha mguu na kichwa chake.


Footy anasimama. Anaangalia tiketi yake, kisha anaangalia Grobb tena.



Mchezaji mzee maarufu wa Soka akawapita, akielekea kutoa maoni kuhusu mchezo huo. “Nisaidie...” Grobb anaomba.

"Sio shida yangu," anasema, akiondoka. Muda huohuo, mlinzi anapita. Grobb ananyosha mkono. “Tafadhali...”

Mlinzi anakunja uso. "Hukupaswa kuwa unasababisha matatizo hapo awali," ananung’unika. Footy anaangalia tiketi yake tena, hii ni moja ya michezo kubwa kuwahi kutokea! Lakini Grobb ameumia...




...Footy anapumua. "Njoo, Grobb," anasema, "hebu twende ukasaidike."

Akionyesha tiketi yake kwa wafanyikazi kwenye lango, ana uwezo wa kumbeba Grobb hadi uwanjani. Grobb ni mzito, na inachukua muda Footy kumbeba hadi maeneo ya matibabu. Anaweza kusikia umati ukishangilia kwa mechi inasikika kua mchezo nzuri! Msimamizi wa matibabu anamwangalia Grobb, kisha Footy. "Unakosa kuona fainali kwa sababu ya kijana huyu? Nilimwona apoawali kikusukuma sukuma ..." Footy anatingiza kichwa. "Ndio, anahitaji msaada..."


"Ah-asante, F-Footy ..." anasema Grobb.

"Footy, eh?" anatabasamu daktari.




Muda mfupi baadaye, kifundo cha mguu cha Grobb kikafungwa. Wakati huo huo, sauti inasikika juu kwa kipaza sauti: Kijana Footy tafathali kuja hapa mahali pa kukusanyika. "Je! Ni nini kinachoendelea?

Msimamizi anapeleka Footy mahali pale - na anashtuka kumwona Bwana Gabba na mwanawe, Jerro, wakimsubiri! Bwana Gabba ndiye mmiliki wa uwanja huo na mtu muhimu zaidi katika Soccatown.



'Tumesikia ulichofanya,' bwana Gabba anatabasamu. 'Ulitoa tiketi yako ili kumsaidia mtu ambaye hata hakukujali.'

Anamkabidhi Footy tiketi mpya kabisa. 'Njoo pamoja nami.' Hii ni tiketi ya kukurusu uweze kuwa upande ya watu muhimu zaidi!



Footy anapata kutazama mchezo uliosalia kutoka kwa mwonekano bora zaidi na pia kuna chakula kizuri cha kula! Jerro anatabasamu. "Umeonyesha moyo wa mchezaji hodari, Footy. Ninajivunia wewe."

Kipindi cha pili kinakaribia kuanza na ni mechi bora zaidi ambayo Footy amewahi kuona!

# MSAMARIA MWEMA




Siku moja mwanasheria mmoja alimwendea Yesu na kumuuliza, "Mwalimu, nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?" Yesu alimuuliza mtu huyo Sheria neno la Mungu linasema nini.

Yule mtu akajibu, "Mpende Mungu kwa moyo wako wote, roho yako yote, akili yako yote na kwa nguvu zako zote na mpenda jirani yako kama jinsi unavyo jipenda" Yesu alimwambia amesema ukweli. Mwanasheria, alitaka kuthibitisha, akauliza, "Jirani yangu ni nani?". Huenda alitarajia Yesu aseme familia au marafiki. Badala yake, Bwana alisimulia hadithi ya kushangaza...



Wakati fulani kulikuwa na mtu aliyekuwa akisafiri kutoka Jerusalemu kwenda Jeriko. Hiyo barabara ilikuwa hatari, ilipinda-pinda katika maeneo yenye miamba ambapo mara nyingi majambazi walijificha. Hakika mtu huyo alipokuwa anatembea, alishambuliwa!


Majambazi hao walimpiga vibaya, wakamwibia vitu vyake na kumwacha amelala kando ya barabara akiwa amejeruhiwa vibaya sana!



Baada ya masaa kupita kuhani alipitia hapo - makuhani walifanya kazi katika hekalu na walijua sheria ya Mungu vizuri sana.

Hakika angesaidia! Lakini kuhani alipomwona mtu huyo aliyejeruhiwa, alivuka upande mwingine wa barabara na kuelekea zake. Kisha akaja Mlawi, mtu mwingine wa kidini. Pia alijua sheria ya Mungu vizuri. Lakini badala ya kusimama ili kusaidia, yeye pia alipita upande mwingine na kuelekea!


Labda alikuwa na shughuli nyingi, au labda aliogopa - lakini kwa hayo yote, alimwacha mtu huyo amelala barabarani.



Hatimaye, Msamaria akaja.

Wasamaria na Wayahudi hawakuwa na huusiano nzuri. Kwa kweli, mara nyingi walikuwa maadui! Hakika Msamaria angempuuza mtu huyo pia...

...hapana! Msamaria hakuweza kumwacha mtu aliyejeruhiwa barabarani. Msamaria huyo alipiga magoti, akasafisha vidonda vya mtu huyo kwa mafuta na divai, na kuvifunga.



Kisha akampandisha mtu huyo juu ya punda wake, akampeleka kwenye nyumba ya wageni, akamtunza.

Siku iliyofuata, Msamaria huyo alimpa mwenye nyumba ya wageni pesa na kusema, "Mtunze vizuri. Nitakaporudi, nitalipia gharama zote za ziada."


Hii ilikuwa fadhili ya ajabu! Msamaria hakusimama tu na kusaidia, bali alijitahidi kuhakikisha kwamba mtu huyo anatunzwa kikamilifu!



Yesu alimuuliza mwanasheria, "Unafikiri ni yupi kati ya hawa watatu alikuwa jirani yake yule aliyejeruhiwa?"

Akajibu "Ni Yule aliyemuonea huruma."


"Nenda ukafanye vivyo hivyo," Yesu akasema.



Kama mwanasheria huyu, watu wengi hufikiria kwamba kufika mbinguni ni lazima ufanya mambo mazuri mingi ya kutosha.

Wanaamini kwamba ukiwa na wema wa kutosha, msaidizi wa kutosha, au kufuata sheria za kutosha, tunaweza kupata njia yetu kwa Mungu. Lakini ukweli ni kwamba, hakuna mtu anayeweza kupata uzima wa milele kwa kuwa ' na wema wa kutosha.' Hatujampenda Mungu kwa moyo wetu wote, roho, akili na nguvu zetu zote, na hatujawapenda majirani zetu kama tunavyo jipenda!

Sisi ni kama huyo mtu aliyejeruhiwa katika hadithi: tumepotea, tumevunjika, na hatuwezi kujiokoa...



...Lakini Yesu ni kama Msamaria Mwema. Ingawa sisi ni wenye dhambi - kwa kawaida ni maadui zake - alitupenda sana hata alitoa maisha yake ili kutuokoa!

Alilipa gharama ya dhambi zetu ili tuweze kusamehewa na kufanywa haki na Mungu tunapoweka tumaini letu kwake! Kwa sababu Yesu ametuonyesha upendo wa ajabu sana, anatuita tuwapende wengine pia - hata watu ambao huenda hatuelewani nao au ambao ni watofauti na sisi.

Kuwa jirani mwema sio tu  kusaidia wale tunaowajua na kuwapenda, lakini ni kuonyesha wema na kumtunza yeyote anayehitaji.

# KULINGANISHA HADITHI

JE, UNAWEZA KULINGANISHA HADITHI YA BIBLIA NA HADITHI YA SOKA?

| HADITHI YA SOKA | HADITHI YA BIBLIA |
| --- | --- |
| 1 GROBB, MMOJA WA WATOTO WAGENI, AMEJERUHIWA VIBAYA. | MSAMARIA ANASIMAMA ILI KUMSAIDIA MSAFIRI HUYO, INGAWA WAO NI ADUI WA WAISRAELI! |
| 2 MWANASOKA MAARUFU ANAMPUUZA GROBB, ANAMPITA. | YESU ANAHESHIMU KIELELEZO CHA MSAMARIA NA ANATUTIA MOYO TUWE KAMA YEYE. |
| 3 MLINZI ANAKATAA KUMSAIDIA GROBB, PIA ANAMPITA. | MSAFIRI ANAPIGWA NA KUACHWA MAUTUTI. 1 |
| 4 FOOTY ANAMSAIDIA GROBB, INGAWA GROBB HAKUWA MWEMA KWAKE. | MLAWI PIA ANAMPUUZA MTU ALIYEJERUHIWA, AKAMPITA. |
| 5 FOOTY ANAJINYIMA NAFASI YAKE YA KUTAZAMA MCHEZO ILI KUPATA USAIDIZI WA KIMATIBABU WA GROBB. | MSAMARIA ANATUMIA PESA NA WAKATI WAKE KUMTUNZA MTU ALIYEJERUHIWA. |
| 6 KUTOKUWA NA UBINAFSI KWA FOOTY KUNATAMBULIWA NA BW. GABBA NA JERRO, NA ANAHESHIMIWA KWA WEMA WAKE! | KUHANI ANAVUKA UPANDE MWINGINE WA BARABARA ILI KUMKWEPA MTU ALIYEJERUHIWA. |





# SOMO LA KUZINGATIA 1 JIRANI YANGU NI NANI?

## Matayarisho

S *Katika hadithi ya soka, ni nani aliyempita Grobb akiwana amejeruhiwa bila kusaidia?*

S *Katika mfano wa Yesu, ni watu gani waliompuuza msafiri aliyejeruhiwa?*

## Majadiliano ya Timu

Jaribu kusimulia Hadithi ya Soka kwa dakika moja. Sasa jaribu kusimulia hadithi ya Biblia pia kwa wakati mmoja!

Je, ni vitafunio gani unavyopenda zaidi? Je, ungeshiriki na nani? Ni nani ambaye haugependa kushiriki naye? Ni rahisi kuwa mkarimu kwa marafiki zetu na watu tunaowapenda, lakini ni vigumu kwa wale ambao wanatuudhi. Yesu anasema bado atahao ni jirani zetu!

## Mafunzo - Mstari wa Kumbukumbu

**Marko 12:31b (NIV) '...Mpende jirani yako kama vile unajipenda.'**

# MPANGO WA MCHEZO WA MUNGU

1

Mara nyingi tunaona utofauti, lakini Mungu hana mapendelio. Kila mtu ni wa thamani Kwake!

**SOMA 1 Samweli 6:7b** 'Bwana haangalii mambo ambayo watu huyatazama. Watu hutazama sura ya nje, lakini Bwana huutazama moyo.'

S ***Tunawezaje kujifunza kuwaona watu jinsi Mungu anavyowaona?***

2

Yesu alionyesha wazi kwamba 'jirani' yetu ni mtu yeyote anayehitaji msaada, hata akiwa ni mtofauti na sisi!

**SOMA Luka 10:36, 37b (NIV)** 'Unadhani ni nani kati ya hawa watatu aliyekuwa jirani yake yule mtu aliyeangukia mikononi mwa wakora?... Yule aliyemrehemu...'

S ***Kwa nini Yesu alimchagua Msamaria kuwa jirani mwema katika hadithi?***

3

Upendo ni zaidi ya maneno – lazima iwena matendo.

**SOMA 1 Yohana 3:18 (NLT)** Wapendwa, tusiseme tu kwamba tunapendana; tuonyeshe ukweli kwa matendo yetu.

S ***Ni njia moja gani  unaweza kubadilisha maneno kuwa vitendo wiki hii?***

✓

***Funga macho yako. Fikiria mtu ambaye ni vigumu kwako kumpenda. Waone wakiwa wamekaa pekeyao na huzuni. Sasa jione ukiwasaidia badala ya kuwaondokea. Hivyo ndivyo Yesu anatuita tufanye - kuwapenda jirani zetu na kuonyesha upendo wa Mungu kwa vitendo kwa wale wanaotuzunguka!***

# KWENDA KWA LENGO

**OMBA:** Mwombe Mungu akusaidie kuwaona watu kupitia macho yake na uwapende hata wale unaowaona wagumu.

**FANYA:** Tafuta nafasi moja wiki hii ili kusaidia au kumtia moyo mtu ambaye kwa kawaida huelewani naye.

**MWAMBIE:** Ambia rafiki yako kwamba Yesu anasema kila mtu ni jirani yako.





# SOMO LA KUZINGATIA 2 GHARAMA YA HURUMA

## Matayarisho

- *Ni nini Footy aliwacha kufanya ili Grobb apate msaada?*
- *Msamaria alimtunzaje mtu aliyejeruhiwa?*
- *Kwa nini wakati mwingine ni vigumu kuacha mambo yako kwa ajili ya wengine?*

## Majadiliano ya Timu

Je, unaweza kufikiria wakati ambapo mtu fulani alishiriki nawewe jambo fulani, hata kama lilimgharimu? Hii inaweza kuwa wakati, pesa, chakula, au kitu chochote kingine. Je, ilikufanya uhisi aje?

## Mafunzo - Mstari wa Kumbukumbu

**Yohana 15:13 Hakuna upendo mkuu kuliko mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake.**

# MPANGO WA MCHEZO WA MUNGU

**1**

Footy alitoa tiketi yake ya dhahabu, na Msamaria akatoa wakati wake na pesa zake. Upendo sio tu juu ya hisia – ina husu dhabihu. Hivyo ndivyo Yesu pia alionyesha upendo wake kwetu.

**SOMA 1 Yohana 3:16 (NIV)** Hivi ndivyo tunajua upendo ni nini: Yesu Kristo alitoa uhai wake kwa ajili yetu.

S ***Kwa nini upendo wa kweli uonekana vyema zaidi inapogharimika?***

**2**

Tunapowajali wengine, inamaanisha kutanguliza mahitaji yao kuliko yetu.

**SOMA Wafilipi 2:3-4 (NLT)** Uwe mnyenyekevu, ukiwafikiria wengine kuwa bora kuliko wewe mwenyewe. Usiangalie masilahi yako tu, bali pendezwa na wengine pia.

S ***Je, ingekuwaje kwako kuwafikiria wengine kuwa bora kukuliko wewe mwenyewe, na kuwajali?***

**3**

Mungu anaona kila tendo la upendo kwa wengine - hata yale madogo!

**SOMA Mathayo 10:42 (NLT)** 'Na ukimpa hata kikombe cha maji baridi kwa mmoja wa walio wadogo katika wafuasi wangu, bila shaka utalipwa.

S ***Ni tendo gani dogo la fadhili unaweza kufanya wiki hii ambalo linaweza kuwa na maana kubwa kwa mtu***

✓ ***Funga macho yako. Hebu wazia umeshikilia kitu unachopenda sana - labda zawadi au tiketi maalum. Sasa fikiria unaiwacha ili mtu mwingine apate kile anachohitaji. Hiyo inaonekana kua ngumu, sivyo? Lakini hivyo ndivyo upendo unafaa kua. Upendo unagharimu kitu - na Yesu alituonyesha upendo mkuu kuliko wote.***

# KWENDA KWA LENGO

**OMBA:** Mshukuru Yesu kwa kutoa maisha yake kwa ajili yako, na umwoombe akusaidie kuwa mkarimu.

**FANYA:** Patiana kitu wiki hii ambacho ni chamaana kwako.

**MWAMBIE:** Mwambie rafiki kwamba upendo si maneno tu - unaonekana katika kile tunachotoa na kufanya.



# SOMO LA KUZINGATIA 3 YESU, MSAMARIA WETU MWEMA

## Matayarisho

- *Je, unaweza kukumbuka ni wapi msafiri katika hadithi ya Yesu alikuwa akisafiri kutoka na kwenda?*
- *Ni mnyama gani alikuwa wa Msamaria?*
- *Je, unaweza kueleza 'dhambi' ni nini? Dhambi ni kitu chochote tunachofikiri, kusema, au kufanya ambacho kinaenda kinyume na njia ya Mungu.*

## Majadiliano ya Timu

Hebu wazia mtu anayezama kwenye kina kirefu cha maji. Je, wanaweza kujiokoa? Hapana! Wanahitaji mtu wa kuwaokoa.

Chukua dakika moja kutaja kazi za uokoaji unazoweza kufikiria.

## Mafunzo - Mstari wa Kumbukumbu

**Warumi 5:8 (NIV) Lakini Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi katika hili: Tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu.**

# MPANGO WA MCHEZO WA MUNGU

1

Kama vile yule mtu aliyelala njiani, sisi hatuna uwezo kwa sababu ya dhambi. Hatuwezi kurekebisha peke yetu.

**SOMA Waefeso 2:1 (NLT)** Mlikuwa wafu kwa sababu ya uasi na dhambi zenu nyingi.

S ***Unafikiri inamaanisha nini kuwa 'wafu' kiroho?***

2

Msamaria huyo alimsaidia mtu ambaye kwa kawaida angekuwa adui yake. Yesu alifanya hata zaidi - Alitoa uhai Wake kwa ajili yetu tulipokuwa tungali maadui wa Mungu.

**SOMA Warumi 5:10b (NLT)** Urafiki wetu pamoja na Mungu ulirejeshwa kwa kifo cha Mwana wake tulipokuwa tungali adui zake…

S ***Unajisikiaje kujua kwamba Yesu alitupenda hata tulipokuwa kinyume Naye?***

3

Kifo cha Yesu kilitufungulia mlango wa kuwa marafiki wa Mungu...

**SOMA 1 Petro 2:24 (NLT)** Yeye binafsi alibeba dhambi zetu katika mwili wake msalabani ili tuwe wafu kwa dhambi na kuishi kwa haki. Kwa majeraha yake mmeponywa.

Yesu alibeba dhambi zetu ili tuweze kutoka kuwa 'wafu KATIKA dhambi' hadi 'wafu KWA dhambi'. Yesu anatuletea msamaha na uzima!

✓

***Funga macho yako. Hebu wazia umelala barabarani, unaumia na hauwezi kuamka. Kila mtu mwingine anapita na kukuacha hapo. Sasa ona Yesu akija kwako. Anapiga magoti, anakuinua, na kukupeleka kwenye usalama. Hivyo ndivyo alivyofanya pale msalabani - alichukua dhambi zetu na adhabu ili tuweze kusamehewa. Ikiwa bado hujamwamini Yesu, unaweza kumwamini hivyo leo - mwambie akusamehe dhambi zako, mshukuru kwa kufa kwa ajili yako, na umwombe awe Mwokozi wako.***

# KWENDA KWA LENGO

**OMBA:** Mshukuru Yesu kwa kukukomboa kutoka katika dhambi na kukupa maisha mapya.

**FANYA:** Onyesha upendo wa Kristo kwa mtu ambaye hataraji wiki hii.

**MWAMBIE:** Mwambie rafiki yako kwamba Yesu alikuja kutuokoa wakati hatukuweza kujiokoa.





# SOMO LA KUZINGATIA 4 NENDA NA UFANYE HIVYO...

## MATAYARISHO

*Je, Footy aliheshimiwa aje baada ya kumsaidia Grobb?*

*Yesu alisimulia hadithi hiyo kwa nani?*

## MAJADILIANO YA TIMU

Ni jambo gani zuri zaidi ambayo mtu amewahi kukufanyia? Je, ilikufanya uhisi aje?

Ni jambo gani zuri zaidi umewahi kumfanyia mtu mwingine? Walionyeshaje shukrani zao?

## MAFUNZO - MSTARI WA KUMBUKUMBU

**Waefeso 4:32 (NIV) Tuweni wafadhili na wenye huruma mmoja kwa mwingine, kusameheana kama vile Kristo Mungu alivyowasamehe nyinyi.**

# GOD'S GAME PLAN

**1**

Yesu hakufundisha tu upendo - aliishi! Aliosha miguu ya wanafunzi wake, akawaponya wagonjwa, akawasamehe adui zake, na kuutoa maisha yake. Tumeitwa kutembea katika nyayo zake.

**SOMA Yohana 13:15 (NIV)** "Nimewawekea kielelezo, ili mfanye kama mimi nilivyowafanyia."

**S** ***Ni baadhi ya njia zipi ambazo Yesu alionyesha upendo ambazo tunaweza kuiga?***

**2**

Ni rahisi kuwa mwema kwa marafiki, lakini je watu wengine?

**SOMA Luka 6:27-28 (NIV)** "Lakini nyinyi mnaosikia nawaambieni, Wapendeni adui zenu, watendeeni mema wale wanaowachukia, wabariki wale wanaowalaani, waombeeni wanaowadhulumu..."

**S** ***Ni kwa nini kuna nguvu zaidi kupenda watu wasio wema kwetu?***

**3**

Katika hadithi ya soka, Footy aliheshimiwa kwa kumsaidia Grobb. Tunapowapenda wengine na kufanya matendo mema, Mungu anapata heshima!

**SOMA Mathayo 5:16 (NLT)** "Kwangia hiyo hiyo, wacha matendo yenu mema na yang'ae ili watu wote wapate kuona, ili kila mtu amsifu Baba yenu wa mbinguni."

**S** ***Je ni kwa nini wema kama wa Kristo unawaelekeza watu kwa Mungu?***

✓

***Funga macho yako. Hebu wazia umeshika tochi kwenye chumba chenye giza. Unapowasha tochi, giza inatoweka. Hicho ndicho kinachotokea tunapoishi na upendo wa Yesu - wema wetu unaangaza nuru yake katika ulimwengu wa giza. Ikiwa unamjua Yesu, mwombe akusaidie kung'aa vyema wiki hii. Na ikiwa bado hauja mkubali Yesu, leo ni siku yako ya kumwamini, ili nuru yake iweze kung'aa ndani yako pia.***

# KWENDA KWA LENGO

**OMBA:** Mwombe Mungu akusaidie kuwapenda watu kama Yesu, hata ikiwa ni vigumu.

**FANYA:** Chagua mtu mmoja wiki hii - labda mtu ambaye huelewani naye - na umfanyie jambo ngema.

**MWAMBIE:** Mwambie rafiki yako kwamba tunaweza kuwapenda adui zetu kwa sababu Yesu alitupenda sisi kwanza.

# AYA YA KUMBUKUMBU

Angalia kama unaweza kujifunza mstari huu!

**Marko 12:31b (NIV)** **'...Mpende jirani yako kama unavyo jipenda.'**

**Warumi 5:8 (NIV)** **Lakini Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi katika hili: Tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu.**

# SOMO MAMBO MUHIMU

- Kila mtu ni jirani yangu! Mungu anatuita tuwapende watu wote, si marafiki zetu tu.
- Upendo wa kweli hughamika kitu - huruma ya kweli inamaanisha kuwaweka wengine mbele yetu wenyewe.
- Yesu ni Msamaria wetu Mwema. Sisi ni wanyonge katika dhambi, lakini alituokoa kwa kufa badala yetu.
- Tumeitwa kupenda kama Yesu. Kuonyesha wema, hata kwa watu ambao ni wagumu kuwapenda.
- Upendo wetu huangaza nuru yake. Tunapoishi vitofauti, watu wanamwona Yesu ndani yetu!